**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015)

*Mary K. Njeru[1], Prof. John M. Kobia, PhD[1] na Dkt. Dorcas M. Musyimi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109 - 60400, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-1020-1650; Barua pepe ya mawasiliano: mariashan4@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*10 Juni 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Usawiri, Motifu, Uhakiki, Tamthilia, Ekolojia, Mazingira asilia.*

**IKISIRI**

Suala la kuongezeka kwa viwango vya halijoto na mabadiliko ya tabianchi limeibua mijadala ya kitaifa na kimataifa. Kwa msingi huu, kazi mbalimbali za kifasihi zimebuniwa kwa kuangazia uharibifu wa mazingira asilia na athari zake na mwito wa kuhifadhi mazingira. Makala hii ilikusudia kuchunguza jinsi motifu za kimazingira zilivyosawiriwa katika tamthilia ya Majira ya Utasa (Arege, 2015). Msisitizo ulikuwa kuangazia jinsi mwandishi wa tamthilia teule amesawiri motifu za kimazingira ili kuonyesha uharibifu wa mazingira pamoja na matatizo yanayotokana na uharibifu huo. Hii ni kwa sababu fasihi huwasilisha hali, maingiliano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira. Kwa hivyo, ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayokumba jamii yoyote iwayo. Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996). Kimsingi, nadharia ya uhakiki wa kiekolojia hujikita katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa kuonyesha uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira. Tamthilia iliyohakikiwa iliteuliwa kimakusudi kwa kuwa maudhui yake makuu yanahusiana moja kwa moja na mada ya makala hii. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia usomaji wa kina wa tamthilia teule. Matokeo ya makala hii yalithibitisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya Majira ya Utasa amesawiri motifu za kimazingira kwa namna mbalimbali kwa kuonyesha njia za uharibifu wa mazingira na athari zake. Hivyo, kushadidia kuwa fasihi inaakisi kikamilifu matatizo yanayoibuka katika jamii ilimoibuka. Kwa hivyo, ni chombo madhubuti kinachoweza kutumiwa kutatua matatizo hayo.

**APA CITATION**

Njeru, M. K., Kobia, J. M & Musyimi, D. M. (2022). Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 151-160. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**CHICAGO CITATION**

Njeru, Mary K., John M. Kobia, & Dorcas M. Musyimi. 2022. "Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015)". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 151-160. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699.

**HARVARD CITATION**

Njeru, M. K., Kobia, J. M & Musyimi, D. M. (2022) "Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015)", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 151-160. doi: 10.37284/jammk.5.1.699.

**IEEE CITATION**

M. K. Njeru, J. M. Kobia & D. M. Musyimi, "Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015)", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 151-160, Jun. 2022.

**MLA CITATION**

Njeru, Mary K., John M. Kobia, & Dorcas M. Musyimi "Usawiri wa Motifu za Kimazingira Katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015)". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Jun. 2022, pp. 151-160, doi:10.37284/jammk.5.1.699.

## UTANGULIZI

Mazingira asilia ni sehemu muhimu katika maisha ya mwanadamu pamoja na viumbe wengine duniani. Aidha, rasilimali ya mazingira huchangia moja kwa moja katika ukuzaji wa uchumi wa taifa kwa kukuza mapato na uzalishaji wa mali. Kwa msingi huu, mazingira safi na yenye kuboresha afya ni kiungo muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo ya Kenya kwenye mpango wa Dira 2030 (Sera ya Kitaifa ya Mazingira, 2012).

Mazingira ni muhimu katika uundaji wa mandhari ya kifasihi. Hii ni kwa sababu mazingira ndiyo huipa kazi ya sanaa usanii na ujumi wake. Kulingana na Buell (2005), sitiari nyingi za kifasihi huzalika kutokana na mazingira ya msanii. Mawazo ya Buell (keshatajwa) yanashabihiana na ya Sangili (2015) anayetambua kuwa baadhi ya misamiati katika kazi za sanaa hasa fasihi hutokana na miti, wanyama, wadudu na mito. Kwa hivyo, ari ya kudhamini mazingira kwa wanajamii inaweza kukuzwa kupitia kazi za fasihi zinazohusu mazingira.

Miongoni mwa mambo yanayotishia kuangamiza mazingira asilia duniani ni pamoja na ufyekaji wa misitu, uchafuzi wa mazingira baharini na nchi kavu na uchafuzi wa maji na hewa (Garrard, 2004). Juhudi katika kuangazia masuala ya mazingira kwa muda mrefu zimekuwa zinahusisha wanaharakati wa kimazingira, wanasayansi mazingira, wanamisitu pamoja na serikali kuu za mataifa mbalimbali duniani (Sangili, 2015). Hii ina maana kwamba hoja na ushahidi wa sayansi asilia kuhusu uharibifu wa mazingira na athari zake vimepewa nafasi kubwa kuliko hoja za sayansi za jamii pakiwemo lugha na fasihi.

Fasihi ya Kiswahili ni mojawapo ya fasihi ambazo zimehusika katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kijamii (Sabula na Sangili, 2019). Miongoni mwa maudhui ambayo yanashughulikiwa na kupewa kipau mbele ni suala la mazingira. Hii inatokana na sababu kuwa fasihi ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii yoyote ile. Aidha, fasihi inaakisi kikamilifu masuala ya jamii ilimoibuka, na inaweza kutumika katika kusuluhisha matatizo ya kijamii.

### Dhana ya Fasihi Mazingira

Fasihi mazingira ni uwanja ulioendelezwa na Glotfelty na Fromm (1996) na Buell (1996) miaka ya 1990 walipozindua tena uwanja wa fasihi mazingira katika fasihi za Kiingereza huko Marekani (Sabula na Sangili, 2019). Vilevile, wanatambua kuwa uwanja wa fasihi mazingira unachukua mkabala wa kimazingira katika masuala ya kifasihi hasa kwa kuchanganua maudhui ya kiekolojia na jinsi wahusika wanavyohusiana na ekolojia.

Fasihi mazingira huwa na kusudi la kuleta mageuzi ya kijamii na kimazingira kupitia fasihi. Kwa hivyo, kando na mazingira asilia, huhusisha mandhari yaliyojengwa na binadamu pamoja na mahusiano yake na utamaduni (Rueckert, 1978). Kinachodhihirika ni kwamba fasihi mazingira ni usomaji wa matini za kifasihi unaoegemea kwenye masuala ya kimazingira. Aidha, uwanja wa fasihi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

mazingira unachukua mwelekeo wa kimwingilianotaaluma kwa kuhusisha falsafa kimazingira, usomi wa mandhari, mapisi kimazingira, nyanda na sehemu za dunia na kuoanisha na sanaa mbalimbali (Rigby, 2002). Uwanja wa fasihi mazingira ulichipuka kutokana na uhusiano kati ya fasihi na mazingira (Buell, 2005). Jinsi mazingira yanavyobadilika ndivyo fasihi inavyoendelea kubadilika kimaudhui huku ikichukua dhima mpya ya kusawiri uharibifu wa mazingira, athari zake na njia za kuhifadhi mazingira ili kuepuka majanga (Wesonga na wenziwe, 2020).

## Dhana ya Motifu katika Fasihi

Dhana ya motifu hutumiwa kurejelea wazo kuu na sehemu ya dhamira katika kazi ya kifasihi (Wamitila, 2003). Huweza pia kutumiwa kuelezea elementi fulani ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani. Umuhimu wa motifu anaoueleza Wamitila (keshatajwa) kwa kuzingatia maudhui na muundo unamaanisha kwamba, kuwapo kwa motifu katika kazi ya fasihi ndiko kunakobeba muundo na maana ya kazi hiyo. Motifu hiyo haiwezi ikaondolewa kwani itaathiri muundo na ujumbe au hata maana ya hadithi. Aidha, Motifu ni kipengele cha kijadi kinachohusu kurudiwarudiwa kwa wazo au dhamira fulani katika sehemu kubwa ya kazi za fasihi hususan riwaya, tamthilia, ushairi, fasihi simulizi na kadhalika (Mulokozi, 2017). Kwa maoni ya Mulokozi (keshatajwa), motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa motifu katika kazi za fasihi, aidha kwa kukusudia au bila kukusudia, waandishi wengi wa kazi za fasihi wamekuwa wakijumuisha motifu katika uandishi wa kazi zao.

## Kiunzi cha Nadharia

Makala hii iliongozwa na nadharia ya uhakiki wa kiekolojia iliyoasisiwa na Glotferty (1996). Nadharia hii ilianza huko Marekani ili kuhusisha wanafasihi katika utetezi wa mazingira, kufuatia mabadiliko ya tabianchi ambayo yalisababishwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika sehemu mbalimbali ulimwenguni (Heise, 2008). Hivyo, harakati ya uhakiki wa kiekolojia ilizuka kutokana na nia ya kuyaboresha mazingira yaliyoangamia, na kuimarisha jinsi mazingira yalivyotendewa na binadamu; mambo ambayo hayakutimika kupitia sayansi, lakini kupitia uandishi na kazi za kifasihi.

Licha ya kuwa tapo hili lilizuka miaka ya tisini, Makala ya Rueckert (1978) `*Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism*` yaliweka msingi uwanja wa uhakiki wa kiekolojia (Barry,2013). Vilevile, Barry (keshatajwa) anatambua makala ya Karl Kroeber (1974) `Home at Grasmere` kama ya kwanza kutumia dhana ya ekolojia katika uhakiki wa kifasihi. Kutokana na maelezo hayo, inadhihirika kuwa uhakiki wa kiekolojia ulibainika katika tafiti za kifasihi kuanzia miaka ya sabini. Kimsingi, Nadharia ya Uhakiki wa kiekolojia huchambua kazi za kifasihi kwa kuangazia vipengele vya uhusiano na utegemeano baina ya binadamu na mazingira. Uhakiki wa kiekolojia ni mkabala wa uchambuzi wa kazi za fasihi ambao huchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na mazingira (Mulokozi (2017). Hivyo, mkabala wa kiekolojia katika uchambuzi wa kazi za fasihi huchukulia mazingira kama suala la msingi katika uhakiki wake.

Uhakiki wa kiekolojia hutazama jinsi mifumo mbalimbali ya kimazingira inavyofanya kazi ili kukidhi maisha na jinsi mifumo hii inavyoharibiwa na kusababisha vifo vya mimea na wanyama (Glotferty, 1996). Matendo kama vile: kukata miti, kujenga nyumba katika mahali oevu, kuongezeka kwa teknolojia haribifu ya kisasa na ukosefu wa uongozi adilifu katika masuala ya ekolojia yamesababisha mitandao ya viungahai kudhoofika. Kwa hivyo, ekolojia imo katika hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya kibinafsi ya kibinadamu. Utamaduni wa binadamu na ulimwengu halisi huhusiana na kuathiriana (Heise, 2008). Kimsingi, utamaduni unahusu namna watu wanavyoishi katika maisha yao ya kila siku. Vilevile, uhakiki wa kiekolojia huchunguza jinsi ambavyo binadamu, utamaduni na mazingira wanaathiriana.

## Kumhusu Timothy Arege, Mwandishi wa Tamthilia ya *Majira ya Utasa*

Timothy Arege ni mzaliwa wa Kaunti ya Kisii Magharibi mwa Kenya. Alianza masomo yake mnamo mwaka 1974 katika shule ya Msingi ya Kisii. Aliendelea na masomo yake ya sekondari

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

katika shule ya upili ya Nyansiongo na baadaye akajiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi alikohitimu na Shahada ya Sanaa katika Kiswahili, Sosiolojia na somo la dini ya Kikristu mwaka wa 1994. Mnamo mwaka wa 1998 alipata shahada ya Uzamili (MA) katika taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Mnamo mwaka wa 2012 alipata shahada ya Uzamifu katika chuo hicho hicho cha Nairobi. Mwaka wa 2008/2009 Arege alipata tuzo ya kuwa msomi bora na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki, Kenya. Vilevile, Arege alishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mwaka wa 2011 kwa kazi yake ya tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (2009). Tamthilia nyingine zilizoandikwa na Arege ni *Chamchela*, *Mstahiki Meya* na *Majira ya Utasa*. Kando na tamthilia, Arege ameandika kazi nyingi katika Kiswahili-fasihi na lugha, pakiwemo mashairi na hadithi fupi. Kwa sasa ni mhadhiri wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

## Uchambuzi wa Tamthilia ya *Majira ya Utasa*

Tamthilia ya *Majira ya Utasa* (Arege, 2015) inahusu jinsi Jumbe, kiongozi anayemiliki mashamba na viwanda vya maua anageuza nchi anayoiongoza kuwa tasa. Anaharibu mazingira kupitia mambo mbalimbali pakiwemo ukataji wa misitu, jambo linaloathiri vyanzo vya maji pamoja na kuachilia kemikali hatari kutoka katika viwanda vya maua kupitia ardhini, mitoni hadi baharini. Vilevile, tamthilia hii inatufunulia jinsi juhudi za wananchi waliozinduka na kuungana kwa kukerwa na uongozi potovu wa Jumbe zinaleta mwamko wa harakati za ukombozi. Katika kuangazia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia teule, vipengele vilivyozingatiwa katika makala hii ni motifu ya maji, motifu ya kifo, motifu ya magonjwa na motifu ya ukame.

## Motifu ya Maji

Mwanadamu pamoja na viumbe hai wengine kwa ujumla wanahitaji maji katika maisha yao ya kila siku (Maganga, 2019). Aidha, anaeleza umuhimu wa maji kama vile kutumika kutibu magonjwa kama vile msongo wa mawazo na ugonjwa wa kisukari, kutumika kupikia, kulimia, kusafishia pamoja na kutumika kama makazi ya wanyama wengine wa majini na viumbe hai mbalimbali viishivyo majini. Hata hivyo, Maganga (keshatajwa) anatambua kuwa mbali na kuwepo na vyanzo vingi vya maji, kumekuwepo pia na uharibifu wa vyanzo hivi. Katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*, umuhimu wa maji unadhihirika kupitia mfano huu:

> *Mbawazi: Naona basi tutakuja kuangamizwa na hii njaa. Ardhi tunayo lakini kumbe haizai bila maji.*
>
> *Bi Siwa: Kila kitu hutegemea maji mama. Maji ni uhai*
>
> *Mbawazi: Naona hali hii ikiendelea tutakuja kufa na kuwa karamu ya tai na fisi (Uk. 6).*

Mazungumzo baina ya wahusika Mbawazi na Bi Siwa yanaonyesha kuwa maji ni uhai kwa sababu kila kitu kinayategemea. Kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi wa tamthilia teule, ardhi yao haizai kutokana na ukosefu wa mvua. Hii ndio maana Mbawazi anasema kuwa wao wana ardhi lakini haizai bila maji. Matokeo ya kukosekana mvua ni kiangazi na njaa, hali inayosababisha vifo vya binadamu na viumbe hai wengine. Uhaba wa maji pia unatokana na misitu kukatwa kiholela. Hali hii imesawiriwa na mtunzi wa *Majira ya Utasa* kupitia mfano ufuatao:

> *Bi Siwa: Majuzi ilikuwa habari tofauti na hii. Sasa tuiamini gani?*
>
> *Siwa: Kwani ilikuwa habari gari?*
>
> *Bi Siwa: Kwamba uhaba wa maji umetokana na misitu kukatwa kiholela na chemchemi za maji kuharibiwa.*
>
> *Siwa: Aliyepinga hilo nani? Uyasemayo wewe yamekuwa yakisemwa kwa muda sasa. Na kwa kweli si siri tena. Yalianza kwa wenyewe hao kujigawia ardhi ambayo ilikuwa mwiko watu kujitwalia. Mengine haya yamefuatia baadaye (Uk. 25).*

Mazungumzo baina ya Siwa na mkewe yanathibitisha kuwa, baadhi ya wanajamii wametambua chanzo cha kukosekana kwa maji. Mhusika Siwa anamweleza Bi Siwa ya kwamba licha ya kuwa baadhi ya viongozi katika jamii wamebadili mikondo ya maji hadi mashambani mwao na kuwanyima wao haki ya kupata kuyafaidi, ukataji wa miti pia umechangia pakubwa katika

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

kukosekana kwa maji. Jambo hili linathibitishwa na Matheka (2018) anayesema kuwa wataalamu wa mazingira wanaonya kwamba ukataji wa miti kiholela hasa nchini Kenya kunaangamiza misitu, kukausha vyanzo vya maji na kuathiri hali ya hewa.

Kutokana na umuhimu wa maji, baadhi ya watu katika jamii huyatumia kama vitega uchumi. Mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anathibitisha haya kupitia mhusika Lulu katika dondoo lifuatalo:

> *Lulu: Usiseme hivyo Jumbe. Watu wananung`unika na kukulaumu wewe.*
>
> *Jumbe: Kuhusu nini?*
>
> *Lulu: Kuhusu mambo kadha. Moja kati ya hayo ni kwamba wewe na wenzako mmechukua sehemu za vyanzo vya maji na kuzigeuza kuwa vitega uchumi vyenu. Kuna fununu kuwa nyinyi ndio mliosababisha kiangazi hiki (uk 38).*

Mfano uliotolewa unaonesha kuwa licha ya wanajamii kutambua umuhimu wa maji, kunao wachache ambao wanawanyima wenzao haki ya kuyafaidi kwa matumizi yao ya kimsingi. Hali hii inachangia katika kusababisha kiangazi na hatimaye njaa isiyokadirika. Kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki wa kiekolojia, matatizo ya kiekolojia hutokea pale ambapo shughuli za kibinadamu zinapoharibu uwezo wa kawaida wa dunia kuwezesha uendelevu wa mifumo ya kiekolojia (Glotferlty, 1996). Hivyo, ni wazi kwamba baadhi ya vitendo vya kibinadamu kama vile ukataji wa misitu na kuharibu vyanzo vya maji kunachangia katika uharibifu wa mazingira, jambo ambalo lina athari si haba.

**Motifu ya Kifo**

Mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* ameonyesha kuwa uharibifu wa mazingira unaweza kusababisha vifo vya binadamu pamoja na viumbe hai wengine. Anasema:

> *Bi Siwa: Deka, wewe ni mtu uliyekulia hapa kama sisi. Unafahamu hali ya ukame na njaa inayozidi kukita mizizi kila kukicha. Nashangaa kuwa unaikana…*
>
> *Deka: Ni makosa kusema kuwa naikana hali isiyokuwepo…*
>
> *Bi Siwa: …Umesahau mara kwamba nyanyako mwenyewe amekufa kwa hiyo njaa miaka mitatu iliyopita? (Uk 12).*

Dondoo lililotolewa linathibitisha kuwa njaa kutokana na kiangazi inaweza kusababisha kifo. Bi Siwa anamkumbusha Deka, ambaye ni mfanyikazi wa Kiongozi Jumbe kuwa hali ya wananchi wa kawaida ni mbaya kiasi cha kusababisha vifo. Hali ya ukame katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi imekita mizizi kiasi cha watu pamoja na wanyama kuangamia kwa sababu ya njaa. Hata hivyo, kutokana na maneno ya Bi Siwa, inaelekea kuwa Jumbe anaikana hali hiyo licha ya kuwa yeye ni mwenyeji wa jamii husika. Huu ni mfano wa viongozi wanafiki na wabinafsi ambao hawajali masilahi ya wananchi waliowachagua. Athari za ukame zina uhalisia katika mataifa mengi kote duniani. Nchini Kenya, takriban Wakenya milioni mbili kutoka majimbo 10 wanakabiliwa na ukame, jambo lililopelekea Rais Uhuru Kenyatta kutangaza kuwa ukame ni janga la taifa. Kwa mujibu wa ripoti ya Msalaba Mwekundu, ukame huo umechangiwa na uhaba wa mvua katika miezi ya Oktoba hadi Desemba mwaka 2020 na mwezi Machi hadi Mei 2021 (Idhaa ya Kiswahili, 2021).

Kando na ukame, vifo vilivyosawiriwa na mtunzi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* vimesababishwa na sumu kutokana na kemikali kwenye viwanda vya maua. Hivyo, hali hii inaathiri sio tu binadamu bali pia wanyama hasa waishio mitoni. Mfano ufuatao unadhibitisha:

> *Hori: Una maana sisi wajinga?*
>
> *Deka: Werevu uko wapi? Mngekuwa nao msingekuwa hapa kutatiza juhudi za wenye juhudi ya kujiendeleza na kuwasaidia nyinyi kwa ajira.*
>
> *Dosho: Sisi ni wajinga kwa kutazama mkiharibu mazingira yetu! Ni wajinga wa kunyamaza watu wetu wanapolipwa pesa nane kwa jasho la kutwa! Sisi wajinga? Sisi wajinga maana watu wetu wafa kwa hilo sumu la hema zenu. Ndiyo, sisi wajinga. Wajinga kwa kutazama tu mnaposumisha samaki wetu ambao hutuhasiri sisi hatimaye. (Uk 53).*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

Kutokana na mifano iliyotolewa inabainika kuwa, kifo cha binadamu na viumbe hai wengine katika jamii iliyosawiriwa na mwandishi kinaweza kusababishwa na njaa kutokana na hali mbaya ya kiangazi. Hali kadhalika, vifo vinatokana na sumu kutoka kwenye viwanda vya maua vya Jumbe. Kama anavyoeleza Omar (2017) katika ripoti yake, moja ya kila sita ya vifo milioni tisa vya mapema kote duniani katika mwaka wa 2015 vinaweza kuhusishwa na magonjwa yanayosababishwa na sumu katika hewa au maji. Hivyo, ni wajibu wa kila mja kuwajibika katika uhifadhi wa mazingira ili kuepuka maafa zaidi.

**Motifu ya Ukame**

Ukame ni hali ya hewa ya sehemu fulani inayofanya pakose maji ya kutosha kwa muda mrefu. Ukame unatokea pia pale ambako watu na kilimo wanategemea maji kwa umwagiliaji na vyanzo vya maji vinakauka. Hali ambayo inahatarisha uhai wa mimea, wanyama na watu (Wikipedia, 2018). Mwandishi wa *Majira ya Utasa* amesawiri hali ya ukame unaoathiri watu katika jamii husika. Kutokana na mazungumzo ya wahusika, inadhihirika kuwa ukame unaoshuhudiwa haujakuwepo nyakati za jadi. kumaanisha kuwa hali imekuwa ikizorota kila kuchao. Mazungumzo yafuatayo baina ya Kato na Hori yanadhibitisha:

> *Kato: Joto hili halijawahi kushuhudiwa tangu tutie fahamu. Ndani hapakaliki na nje ni mfano wa tanuu. Huu ni mwaka wa hari.*
>
> *Hori: Kiangazi cha namna hii sijakiona mimi. Nimekuwa nikizisikia hadithi za mbali huko. Hadithi za Sahara na Kalahari. Si hapa kwetu. Viwango hivi vya joto vinaweza kukuyeyusha ubongo ikiwa utalifanyia ushindani.*
>
> *Kato: Makubwa haya! Maisha yetu yamekuwa ni dhiki kwa dhiki.*

Katika mazungumzo hayo, Kato anamwambia Hori kuwa viwango vya joto vinavyowakabili havijawahi kushuhudiwa katika jamii yao. Aidha, Hori anakiri kwamba kwa muda mrefu amekuwa akisikia habari kuhusu kuongezeka kwa viwango vya joto katika sehemu tofauti kama vile Sahara na Kalahari bali si kwao. Hii inamaanisha kwamba janga hili ni geni katika jamii yao. Kutokana na hali hii, maisha yao yamekuwa katika dhiki kuu ya njaa iliyosababishwa na ukame. Maelezo haya yanadhibitishwa na ripoti ya VOA ya Oktoba 2021 kuhusu maafa ya ukame na njaa barani Afrika. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mamilioni ya watu barani Afrika hawana uwezo wa kupata chakula cha kutosha. Kwa mfano, Somalia iko ukingoni mwa janga la njaa. Ukame nchini Kenya umesababisha serikali kutangaza hali ya hatari. Kaskazini Mashariki ya Nigeria inakabiliwa na utapiamlo, na njaa imekwishatangazwa katika baadhi ya sehemu za Sudan Kusini. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa maisha ya watu wengi yako katika hatari ya maangamizi zaidi ikiwa uharibifu wa mazingira hautakomeshwa.

Hata hivyo, viongozi katika mataifa yanayokabiliwa na janga la ukame hawashughuliki licha ya kujua hali ilivyo. Kutokana na mazungumzo baina ya wahusika Dosho na Jumbe, ni wazi kwamba viongozi ndio wamechangia katika uharibifu wa mazingira, jambo ambalo linaadhiri tu wananchi wa kawaida peke yao. Haya yanadhibitika katika mfano ufuatao:

> *Jumbe: Mbona basi wasiridhike? Mbona wasishukuru kwamba nimewaletea ajira mpaka milangoni mwao?*
>
> *Dosho: Kweli ajira ipo ila haitufai. Angalia ukame ulivyokithiri.*
>
> *Jumbe: Unaona? Ukame hauko hapa tu. Duniani kote viwango vya joto na ukame vimeongezeka. Si Jumbe aliyevisababisha. Ndivyo hali ilivyo sasa hivi. (Uk 72).*

Mhusika Jumbe anazungumza na wawakilishi wa wanajamii, Dosho na Mebo anapowaambia kuwa yeye siye aliyesababisha ukame kwani viwango vya joto na ukame viko katika sehemu zote duniani. Akieleza kuhusu athari za uharibifu wa mazingira, Sangili (2015) anasema kuwa athari hizi ziko kote duniani. Anatoa mfano wa mataifa ya Afrika ambapo watu wanaaga kwa njaa, Asia watu wanakufa kutokana na kabobo za *Tsunami*, Marekani wanaangamia kutokana na mafuriko na vilevile Bara Uropa wanaathirika kutokana na joto kali. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba hali ya ukame inaathiri jamii katika sehemu nyingi kote duniani, jambo ambalo linasawiriwa na mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* ili yaangaziwe upya na wote wanaohusika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

Kwa mujibu wa tamthilia teule, hali ya ukame imesababishwa na mambo mbalimbali pakiwemo ukataji miti. Mfano ufuatao unashadidia:

*Kato: Hata madhabahu?*

*Hori: Madhabahu gani? Hamna hata unyasi uliosimama. Mavumbi tu. Watu waliisha kujitwalia wakaikata miti. Tunasikia baadhi baadhi waliiuza ng`ambo. Kuna wakati Mebo alisema kuwa miti iliuzwa na wakubwa kufanyia kampeni. Walipoona limebaki shamba tupu, wakaamua kulifanyia shughuli za kilimo. Sasa matokeo yake haya, kiangazi (Uk 60).*

Katika mfano uliotolewa, mhusika Hori anamweleza Kato kuhusu chanzo cha kiangazi kinachoshuhudiwa katika jamii yao. Kutokana na maneno yake, ni wazi kwamba viongozi walikata miti kiholela na kuiuza ili kufanyia kampeni. Matokeo ya ukataji miti ni kiangazi kinachoshuhudiwa. Kama anavyoeleza Maathai (2009) katika *`The Challenge for Africa`*, rasilimali asilia zingali zinadhulumiwa kupitia shughuli za binadamu kwa kupuuza afya bora ya mazingira. Hivyo, kuenea kwa jangwa kupitia ukataji wa miti kunaathiri vyanzo vya maji, nyanja za kufugia na mashamba kwa ajili ya kilimo na kuchangia katika uchamkaji wa chakula wa dharura.

Hali kadhalika, ni dhahiri kuwa ukame uliokithiri katika jamii umesababishwa na tamaa ya viongozi ya kujilimbikizia mali pamoja na ujinga wa kutotambua athari za matendo yao. Jambo hili ni dhahiri katika jamii ambapo viongozi wanawahadaa wananchi kuwa wangewashughulikia masilahi yao ili waweze kuchaguliwa. Baada ya kuchaguliwa, wao hunyakua mali ya umma huku wakijifaidi wao wenyewe pamoja na marafiki wao wa karibu. Mtunzi anasawiri hali hii kupitia maneno ya mhusika Hori kama ifuatavyo:

*Kato: Kama ni kweli hivyo ulivyosema, ina maana tumevamia makao yao. Sasa naona lililobaki ni sisi kuwawinda kuupigania uhai wetu nao wakituwinda ili kupata chakula.*

*Hori: tumefikia hali ambapo tunawazika watu wetu eti kwa sababu ya njaa. Njaa iliyosabibishwa na ukame. Ukame! Ukame waliousababisha wanadamu. Labda kwa tamaa, labda kwa ujinga (Uk 66).*

Kupitia dondoo hili, inaelekea kuwa mtunzi wa *Majira ya Utasa* anawalaumu viongozi ambao wanachangia katika kuharibu mazingira kwa sababu ya tamaa yao. Kiongozi Jumbe anawakilisha viongozi wa Kiafrika ambao walitwaa ardhi kubwa ya umma na kuvamia maeneo ya misitu. Matokeo ya matendo yao ni uharibifu wa mazingira asilia na hatimaye athari zisizokadirika kama vile njaa kutokana na kiangazi pamoja na kuongezeka kwa viwango vya joto. Utafiti wa Sangili (2015) unashadidia maelezo haya kwa kutambua kuwa viongozi katika serikali huchangia kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa mazingira kwa namna mbalimbali.

Hali ya wanajamii ya kuasi mambo ya jadi inaweza kuwa chanzo cha maafa katika jamii kama vile janga la ukame. Mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* anafafanua haya kupitia mfano ufuatao:

*Deka: Umma uliopo ni mchanganyiko. Hata watoto na wazee wapo. Jumbe: Wazee nao yanawahusu nini?*

*Deka: madhabahu. Wanadai uliharibu madhabahu yao na kuighadhabisha mizimu. Ndiyo maana kuna kiangazi. Nasikia wanataka kuanza kujenga madhabahu. (Uk 81).*

Dondoo lililonukuliwa linaonyesha kuwa kila mwanajamii anapaswa kujukumika katika harakati za kuokoa mazingira yaliyoharibiwa. Hii ndio sababu hata wazee wanajiunga na watoto kulalamikia kuharibiwa kwa madhabahu ambayo walitumia tangu jadi kutoa kafara. Maelezo haya yanaafikiana na matokeo ya utafiti wa Bulaya na Mhango (2020) waliobaini kuwa athari za uchafuzi wa mazingira zinagusa makundi yote ya kijamii pakiwemo watoto. Kwa hivyo, mapambano dhidi yake yanapaswa kuwa jumuishi bila kujali jinsia, umri, elimu, mamlaka au hata uwezo wa kiuchumi alionao mtu. Aidha, kwa mujibu wa Glotferty (1996), uhakiki wa kiekolojia huchunguza jinsi ambavyo binadamu, utamaduni na mazingira wanaathiriana. Kwa msingi huu, inadhihirika kuwa utamaduni wa binadamu huathiri uhusiano wake na mazingira anamoishi. Hivyo, ni wazi kwamba kuna baadhi ya mambo ya jadi mema yanayopaswa kuzingatiwa na jamii ya sasa ili kuepuka majanga yanayokabili jamii husika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

**Motifu ya Magonjwa**

Mtunzi ametumia motifu ya magonjwa kuonyesha athari za uharibifu wa mazingira. Kikohozi cha mhusika Mebo ni dhihirisho la hali mbaya ya wafanyakazi katika viwanda vya maua vya Jumbe. Aidha, mwandishi anatumia motifu ya magonjwa kwa lengo la kusawiri hali inayokumba wafanyikazi katika jamii. Mfano ufuatao unadhibitisha:

> *Mebo: Je, wafanyakazi wako hawakufa katika mazingira hatari bila vifaa vinavyohitajika huku wafahamu kuwa ni kinyume cha sheria na ubinadamu? Je, hukujitwalia ardhi ya umma na kuitumia kujitajirisha? Je, hukuzielekeza sumu hatari mtoni? Tazama! Tulikuchagua wewe tukidhani utatetea na kulinda maslahi yetu. Kumbe sivyo! Umetuua huku unacheka.*
>
> *Jumbe: Watu waliokufa sikuwaua mimi. Wamekufa kwa njaa. Na njaa yenyewe imetokana na ukame. Mimi nina uwezo gani kuzuia ukame. Mimi si Mungu! (Uk 75).*

Kutokana na mazungumzo haya baina ya Mebo na Jumbe, inadhihirika wazi kuwa Jumbe ni kiongozi asiyejali wananchi waliowachagua. Yeye ni kiongozi katili na binafsi ambaye baada ya kuchaguliwa anajitwalia vipande vya ardhi ya umma na kuanzisha viwanda vya maua kwa manufaa yake binafsi. Zaidi ya hayo, wafanyakazi wake wanafanya kazi bila vifaa vinavyohitajika kinyume cha sheria. Hali hii inasababisha magonjwa kama vile kikohozi cha Mebo kisichopona. Pamoja na hayo, anachangia katika kuachilia kemikali mitoni ambayo inahatarisha maisha ya wanyama waishio humo.

Aidha, yaelekea kuwa kando na kuwalipa wafanyikazi mshahara mdogo, Jumbe anawaajiri wafanyikazi bila kuwaaeleza madhara ya kemikali wanazotumia. Baadhi ya wafanyakazi wametambua kuwa wanadhulumiwa ndiposa wanachukua hatua ya kwenda kwa Jumbe ili kumweleza hali yao. Mazungumzo yafuatayo yanashadidia:

> *Dosho: Na usisahau kuwa hata huo ujira uwalipao wafanyakazi wako ni mdogo mno ukilinganishwa na gharama ya maisha.*
>
> *Mebo: Si gharama tu. Hata hasara zake ni kubwa. Mwenyewe bwana Jumbe unafahamu madhara ya kemikali katika shamba lako la maua. Kemikali ile inaua. Watu wamepewa kazi bila kuelezwa hili. Na tayari tumewazika watu sita. Wote wafanyakazi wako. Wote wameuawa na gonjwa la maua. (Uk 73).*

Mfano uliotolewa unahusu mazungumzo baina ya Dosho na Mebo wakimweleza kiongozi Jumbe kuhusu matatizo yanayokumba wanajamii kutokana na uharibifu wa mazingira. Hivyo, Jumbe ni kielelezo cha viongozi ambao wanahatarisha maisha ya wananchi bila kujali. Licha ya Jumbe kujua madhara ya kemikali katika shamba la maua, anawaajiri wafanyakazi bila kuwaeleza. Hii ndio sababu Mebo anasema kuwa ile kemikali inaua kwani tayari wamewazika watu sita, wote wakiwa wafanyakazi wa Jumbe. Dhihirisho kuwa waliathiriwa na kemikali hiyo.

Kando na kikohozi, kemikali imeathiri ngozi za baadhi ya wanajamii hasa watoto. Kutokana na maneno ya mhusika Dosho, watoto wengi wameathiriwa na ugonjwa huu kiasi cha kuzua hofu miongoni mwa wazazi wao. Katika mazungumzo yafuatayo, Dosho anasema:

> *Mebo: Shibe gani Jumbe? Sisi hatulali usiku bwana kwa kukohoa na wewe unadai tumeshiba! Kama tumeshiba ni hii shibe ya kohozi.*
>
> *Dosho: Jumbe, ukweli ni kwamba watu wetu wameteseka. Watu wetu wameumia na wewe unajua japo hutaki kukubali. Watu wetu wanakufa kwa njaa tusiweze kuwasaidia watoto wetu wamo hatarini. Tishio kwa uhai wao ni tishio la kizazi cha mwanadamu. na si hayo tu, tuna mzigo mkubwa kuwalea wagonjwa wa kemikali. Afadhali hili la kukohoa. Wapo walioliwa na kemikali ngozi zao zikabaki nyama. Zimekunwa hadi ya kutokunika tena (Uk 75-76).*

kwa mujibu wa dondoo lililonukuliwa, wapo wanajamii hasa watoto ambao ngozi zao zimeliwa na kemikali kiasi cha kubaki vidonda. Hili ni dhihirisho kwamba kizazi cha baadaye kiko katika hatari ya kuathirika kutokana na uharibifu wa mazingira. Maelezo haya yanashadidiwa na utafiti wa Mutua (2020) anayedai kuwa wanasayansi wametambua uharibifu wa mazingira unaoendelezwa na shughuli za binadamu, kama vile ukataji wa miti, ufyekaji wa misitu kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu na uwindaji wa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

wanyamapori kama mojawapo ya chanzo cha milipuko ya majanga na maradhi. Hii ndio maana mwandishi wa tamthilia ya *Majira ya Utasa* amesawiri athari za uharibifu wa mazingira kwa lengo na kuchochea kila mja kuhusika katika uhifadhi wake.

## Hitimisho

Makala hii imeangazia usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia ya *Majira ya Utasa*. Kutokana na matokeo ya uchunguzi, imebainika kuwa Timothy Arege ametunga kazi hii ili kuangazia matatizo ya jamii ya sasa yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira. Uchanganuzi umeonyesha kuwa mwandishi ametumia motifu za kimazingira mbalimbali ili kuonyesha chanzo na athari za uharibifu wa mazingira. Motifu ya maji imetumika ili kuonyesha umuhimu wa maji kwa binadamu pamoja na viumbe hai wengine. Umuhimu wa maji uliosawiriwa ni kama vile matumizi katika kilimo, kutekeleza usafi, kufugia, kupikia pamoja na kuwa makazi ya baadhi ya wanyama. Vilevile, maji yamesawiriwa kuwa uhai hivi kwamba kila kiumbe kinahitaji maji ili kuishi. Kando na maji kuwa uhai, Arege ameonyesha kuwa vyanzo vya maji vimeharibiwa kupitia vitendo vya binadamu, jambo ambalo limesababisha majanga chungu nzima. Mtunzi ametumia motifu ya kifo kuonyesha athari za uharibifu wa mazingira. kutokana na uchanganuzi, vifo vinavyotokea katika jamii iliyosawiriwa na mtunzi vinatokana ama na njaa au magonjwa. Kutokana na maneno ya baadhi ya wahusika, kufa njaa ni aibu, ndiposa wahusika wanaamua kuungana ili kutetea mazingira yaliyoharibiwa na viongozi wasiojali. Arege amesawiri hali ya ukame iliyokita mizizi katika jamii. Aidha, janga la ukame linaathiri watu katika kila pembe ya dunia. Ukataji wa miti pamoja na kuasi baadhi ya mambo ya kijadi kama vile itikadi ya madhabahu ni miongoni mwa visababishi vya ukame kwa mujibu wa tamthilia ya *Majira ya Utasa*. Aidha, uchunguzi umebaini kuwa vita dhidi ya uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame ni suala linalohusisha kila mwanajamii pakiwemo wazee na watoto. Magonjwa yanayosawiriwa na mtunzi ni kikohozi na ugongwa wa ngozi. Magonjwa haya yamesababishwa na kemikali kutoka katika viwanda vya maua vya kiongozi Jumbe. Aidha, ni dhahiri kuwa mtunzi anawalaumu waajiri ambao huwaajiri wafanyikazi katika viwanda bila kuwaeleza madhara ya baadhi ya kemikali wanazozitumia. Vilevile, anawakashifu waajiri ambao huwaruhusu wafanyakazi wao kufanya kazi bila vifaa vinavyohitajika, kinyume cha sheria. Hivyo, inadhihirika kuwa Arege katika tamthilia ya *Majira ya Utasa* ameangazia chanzo na athari za uharibifu wa mazingira kiubunifu kwa lengo la kuweka wazi matatizo ya jamii yanayotokana na uharibifu huo.

## Marejeleo


Arege, T.M. (2015). *Majira ya Utasa*. Nairobi: Spotlight Publishers (E.A) Limited.

Barry, P. (2013). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester: Manchester University Press.

Buell, L. (2005). *The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Study*. Maldenblackwell Publishers.

Bulaya, J &Mhango, P (2020). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. *Mulika* no. (38) pp105-125

Garrard, G. (2004). *Ecocriticism.* Oxfordshire: Routledge.

Glotfelty, C. & Fromm, H. (1996). *The Ecocriticism Reader: Landmark in Literary Ecology*. Georgia: University of Georgia Press.

Glotferty, C. (1996). *Introduction. The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. Katika Cheryll Glotferty and Harold Fromm. Athens: The University of Georgia Press.

Heise, K. U. (2008). Ecocriticism and the Transnatinal turn in American Studies. *American Literary History* 20(1-2), 381-404.

Idhaa ya Kiswahili (09/09/2021). Rais Kenyatta Atangaza Ukame kuwa Janga la Kitaifa Nchini Kenya. Available at https:/www.google.com/amp/s/amp.dw.com/sw/rais-kenyatta-atangaza-ukame-kuwa-janga-la-kitaifa-kenya/a-59131925: accessed on 05/10/2021.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699

Maathai, W. (2009). *The Challenge for Africa*. Britain: William Heineman.

Maganga, A. G. (2019). Umuhimu wa Maji katika Maisha ya Mwanadamu. Available at http://alexmaganga.blogspot.com/2019/02/umuhimu-wa-maji-katika-maisha-ya-.html?m=1: accessed on 03/10/2021.

Matheka, B. (2018). Hatari Nchi kugeuzwa Jangwa Kufuatia Ukataji wa Miti Kiholele. Available at https://taifaleo.nation.co.ke/?p=2630: Accessed on 05/10/2021.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es salaam: KAUTTU.

Mutua, P. (2020). "Conserve Environment to Avoid Pandemics". Daily Nation, page 18: 02/09/2020.

Rigby, K. (2002). *Ecocriticism in Julian Wolfreys (ed) Introducing Criticism in the twenty-first century*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Rueckert, W. (1978). *Literature and Ecology: An Experimentin Ecocriticism*. Athens: University of Georgia Press.

Sabula, M na Sangili, N. (2019). Fasihi Mazingira: Mtazamo wa Kinisai katika Riwaya ya *Nakuruto*. Koja la Taaluma za Insia. 6(2019): 338-354. Wesonga, E et al (2020). Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule za K. W. Wamitila. East African Journal of Swahili Studies. 2 (2020): 2707-3467.

Ojomo, P. A. (2011). Environmental Ethics: An African understanding *in the Journal of Pan African Studies*, vol 4(3), march 2011.

Omar, F. (2017). Uchafuzi wa Mazingira ni Hatari kuliko Vita na Baa la Njaa. Available at https:www.dw.com/sw/uchafuzi-wa-mazingira-ni-hatari-kuliko-vita-na-baa-la-njaa-utafiti/a-41051751. Accessed on 03/10/2121.

Sangili, N. (2015). Nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika uwanja wa fasihi mazingira. *CHAKAMA* (2015):73-84.

Sera ya Kitaifa ya Mazingira (2012). *Toleo Maarufu ya Sera ya Kitaifa ya Mazingira*. Nairobi: The International Development Institute-Africa (IDIA)

VOA (05/10/2021). Maafa ya Ukame na Njaa. Available https://www.voaswahili.com/maafa-ya-ukame-na-njaa. Accessed on 05/10/2021.

Wesonga, E. et al (2020). Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule za K. W. Wamitila. East African Journal of Swahili Studies. 2 (2020): 2707-3467.

Wikipedia (2018). Ukame. Available at https://sw.m.wikipedia.org/wiki/Ukame: Accessed on 30/09/2021.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.